ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

*Supplement No. 40* *2th October, 2020*

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.40. Vol.101 dated 2th October, 2020*
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 834 la tarehe 2/10/2020

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,

SURA 290

# SHERIA NDOGO

*(zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16 (1))*

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA ZA MWAKA 2020

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba za Mwaka 2020.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba.

tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo:

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;



Scanned by CamScanner

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi.

Utozaji wa ada na ushuru

4.- (1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kanuni ndogo ya (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi zitalipwa kwa Halmashauri.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi.



Scanned by CamScanner

(5) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (4), Halmashauri inaweza kukubaliana na walipa ushuru wakubwa kuweka utaratibu maalum wa kulipa ushuru.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

Muda wa kukusanya ada na ushuru

6.- (1) Muda wa kukusanya ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(4) Malipo ya ada na ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama uthibitisho wa malipo yaliyofanyika.

Usimamizi wa Sheria Ndogo

7.- (1) Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo itafanyika bila ya kuwa na leseni au kibali kinachotolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala wake anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa masharti ya Sheria Ndogo hizi.

(3) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya



Scanned by CamScanner

(2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ada au ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za Mahakama na gharama za mnada.

(4) Wakala hataruhusiwa kukamata mali au bidhaa bila kupata idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo umesababishwa na Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

8.- (1) Halmashauri inaweza kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hizi;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

9. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kwa nia ya kukagua



Scanned by CamScanner

malipo ya ada au makusanyo ya ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Makosa na adhabu

10.- (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na akipatikana na hatia atahukumiwa adhabu isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichopungua miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani kifungo na faini.

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri au shughuli zinazohitaji kulipiwa ushuru.

(2) Mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1) (b) na (c) atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichopungua miezi sita au vyote kwa pamoja kifungo na faini.

Kufililisha kosa

11. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufililisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi kisichopungua laki mbili na kisichozidi laki tano endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Tangazo la Serikali Na. 75 la mwaka 2009

Na Tangazo la

12. Sheria Ndogo zifuatazo za Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba zimefutwa.

(a) Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba (Ada na Ushuru) za mwaka 2009.



Scanned by CamScanner

Serikali No. 146 la mwaka 2004

(b) The Kwimba District Council (Building Mineral fees) of 2004.



Scanned by CamScanner

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ndogo ya 4(1))*

| | |
|---|---|
| SEHEMU YAKWANZA | |
| Ada kwa kukodi au kupanga Majengo ya Halmashauri (Siyo nyumba za Wafanyakazi) | |
| 1. Nyumba za kuishi | Kiasi ambacho kimeainishwa katika mkataba husika |
| 2. Nyumba ya biashara/ofisi | Kiasi ambacho kimeainishwa katika mkataba husika |
| 3. Kodi ya pango ya vibanda vilivyomo katika masoko na stendi za Halmashauri | Shilingi 200,000/= kwa mwaka |
| Ushuru wa meza zilizomo kwenye masoko ya Halmashauri | Shilingi 300 kwa siku au Shilingi 5000 kwa mwezi |
| SEHEMU YA PILI | |
| Ada za huduma za Afya na usafi wa mazingira | |
| 1.Ada ya kupima wahudumu wa nyumba ya kulala wageni, Hotel, Mgahawa, Muuzaji wa vyakula vilivyopikwa au kukaangwa anawajibika kusajili kwa Halmashauri ili kubainisha ukamilishaji wa afya yake kuendelesha shughuli hiyo. | 1. Shilingi 3,000/= kwa kila mtu kwa miezi 6 |
| Ada ya uzoaji taka | |
| Makazi kwa kila kaya | Sh. 1000/= kwa mwezi |
| Viwanda, Mashirika n.k | Sh. 20,000/= kwa mwezi |
| Mgahawa (Cafeteria) -Ndogo | Sh. 1,000/= kwa mwezi |
| Kibanda cha vinywaji baridi | Sh. 1,000/= kwa mwezi |
| Nyumba ya kulala wageni | Sh. 3,000/= kwa mwezi |
| Zahanati binafsi | Sh. 3,000/= kwa mwezi |
| Kituo cha Afya binafsi | Sh. 5,000/= kwa mwezi |
| Hospitali | Sh. 7,000/= kwa mwezi |
| Kiwanda cha mbao (kwa trip) | Sh. 10,000/= kwa mwezi |
| Watengeneza samani (furniture) | Sh. 7,000/= kwa mwezi |
| Garage | Sh. 10,000/= kwa mwezi |
| Car warsh | Sh. 10,000/= kwa mwezi |
| Wafanyabiashara wengineo | Sh. 2,000/= kwa mwezi |
| SEHEMU YA TATU | |
| Ada ya Mabadiliko ya matumizi ya Ardhi | |
| 1. Makazi kuwa biashara | 1. Shilingi 100,000/= |
| 2. Makazi kuwa kiwanda | 2. Shilingi 200,000/= |
| 3. Makazi kuwa Housing estate (biashara n.k. | 3. Shilingi 100,000/= |
| 4. Viwanda/Biashara kuwa kituo cha mafuta. | 4. Shilingi 200,000/= |
| 5. Kugawanya viwanja au shamba | 5. Shilingi 150,000/= |
| 6. Kuhakiki milki | 6. Shilingi 20,000/= kwa kiwanja |
| 7. Aina nyingine ya mabadiliko | 7. Shilingi 50,000/= |
| Ada ya vibali vya ujenzi | |



Scanned by CamScanner

| Ukubwa wa kiwanja - Makazi | Kiwango cha tozo ya Ada |
|---|---|
| 1 – 300m² | Shilingi 30,000 |
| 301 – 600m² | Shilingi 35,000 |
| 601 – 800m² | Shilingi 35,000 |
| 801 – 1000m² | Shilingi 40,000 |
| 1001 – 1500m² | Shilingi 45,000 |
| 1501 na kuendelea | Shilingi 50,000 |
| Hoteli/Guest house | Shilingi 50,000 |
| Taasis i.e shule, chekechea | Shilingi 100,000 |
| Kiwanda- kikubwa | Shilingi 300,000 |
| Kiwanda- kati | Shilingi 200,000 |
| Kiwanda- kidogo | Shilingi 100,000 |
| Ghala (Godwon) | Shilingi 200,000 |
| Kituo cha mafuta | Shilingi 200,000 |
| Karakana | Shilingi 200,000 |
| Minara ya simu | Shilingi 500,000 |
| Car wash | Shilingi 200,000 |
| Ghorofa (floor 1-3) | Shilingi 200,000 |
| Ghorofa (floor 4-5) | Shilingi 300,000 |
| Nyumba ya makazi/biashara | Shilingi 50,000 |
| Taasisi i.e shule,chekechea na n.k | Shilingi 100,000 |
| Nyumba za biashara | Shilingi 100,000 |
| Kiwanda aina zote | Shilingi 200,000 |
| Kituo cha mafuta | Shilingi 200,000 |
| Uzio | Shilingi 100,000 |
| Ukumbi wa burudani au mikutano | Shilingi 200,000 |
| Aina nyingine ambayo haijatajwa | Shilingi 50,000 |

| SEHEMU YA NNE | |
|---|---|
| Ada ya matumizi ya maeneo ya wazi ya Halmashauri | |
| 1. Kibali cha kuweka konteina la biashara eneo la wazi linalomilikiwa na Halmashauri | 1. Shilingi 200,000/= kwa mwaka kwa kila kontena |
| 2. Kibali cha kuweka kiosks eneo la wazi linalomilikiwa na Halmashauri | 2. Shilingi 100,000/= kwa kila mwaka kwa kila kiosks. |
| 3. Fomu ya maombi ya biashara (Kuweka kontena kufungua kiosks n.k eneo la wazi) | 3. Shilingi 15,000/= kwa kila ombi. |

| SEHEMU YA TANO | |
|---|---|
| Ushuru wa Minada | |
| Ushuru wa mnada wa jumla | 1. Kitu chochote kitakachonadiwa kitalipiwa ushuru kiasi cha 2% ya bei ya mnada |
| Ushuru wa minada na magulio ya kila juma ya Halmashauri | 2. Shilingi 1000 kwa kila mfanyabiashara wa bidhaa za viwandani au kilimo |
| | 3. Shilingi 2,000 kwaTenga la kuku |
| | 4.Malori yanayopeleka na kuchukua mizigo mnadani Shilingi 2,000 kwa gari |

| SEHEMU YA SITA |
|---|
| Ada ya kuzingira na kuweka majukwaa katika maeneo ya kati na maeneo mengine (ujenzi, Mikutano n.k). |



Scanned by CamScanner

*Tangazo la Serikali Na.834 (Linaendelea.)*

| | |
|---|---|
| 1.Kwa muda chini ya wiki moja | Shilingi 1000/= kwa kila mita |
| 2. Kwa muda chini ya wiki mbili na usiozidi wiki nne. | 1000/= kwa kila mita |
| 3. Muda zaidi ya wiki 4 na sio zaidi ya 9 | Tshs 4000/= kwa kila mita |
| SEHEMU YA SABA | |
| Ada ya usajili na uchimbaji wa malighafi za madini ya Ujenzi | |
| (a) Ada ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi (Mchanga, kifusi n.k). | Tshs.100,000/= kwa mwaka |
| (b) Usajili wa umiliki wa madini ya kokoto au mawe | Tshs. 150,000/= kwa mwaka |
| Ushuru wa madini ya ujenzi kwa uzito | |
| (a) Mawe | Shilingi 3,000/= kwa kila Trip ya lori lisilizodi Mita 5 za ujazo |
| (b) Kokoto | Shilingi 5,000/= kwa kila Trip ya lori lisilizodi Mita 5 za ujazo |
| (c ) Mchanga | Shilingi 3,000/= kwa kila Trip ya lori lisilizodi Mita 5 za ujazo |
| (c) Moramu | Shilingi 2,000/= kwa kila Trip ya lori lisilizodi Mita 5 za ujazo |
| SEHEMU YA NANE | |
| Ada ya matangazo ya biashara (Promotion) na shughuli za kiutamaduni | |
| (a) Utangazaji wa kibiashara kutumia vipaza sauti kwenye magari madogo | Shilingi. 30,000/= kwa kila Tangazo kwa siku |
| (b) Utangazaji wa biashara kwa kutumia magari makubwa na vikundi vya wasanii (promotion) | Shilingi 50,000 kwa siku |
| (c) Harusi na ngoma za jadi | Shilingi 50,000 kwa wiki moja |
| (d) Kumbi za video na sinema | Shilingi 100,000 kwa mwaka |
| (e) Kumbi za harusi | Shilingi 100,000 kwa mwaka |
| Ada ya matangazo ya biashara yaliyosimikwa kuchorwa kuchapishwa na kubandikwa katika eneo lolote la Halmashauri. | |
| Matangazo yasiyowaka taa (Non – ilamunated) | Shilingi 50,000/= kwa futi 1 ya mraba kwa mwaka |
| Matangazo yenye mwanga (illuminated advertisement) | Shilingi 15,000/= kwa futi 1 ya mraba kwa mwaka |

SEHEMU YA TISA

| | |
|---|---|
| Ada ya Stendi na maegesho yanayomilikiwa na Halmashauri | |
| Maegesho maalum kwa ajili ya Malori ya mizigo | Shilingi 2,000/= kwa siku |
| Mabasi makubwa ya Abiria | Shilingi 3,000 kila yanapotumia stendi |
| Mabasi ya kati Tata/Coaster etc | Shilingi 2,000 kila yanapotumia stendi |
| Hiece | Shilingi 2000 kwa siku |
| Taxi na gari nyingine Ndogo | Shilingi 500 kwa siku |



Scanned by CamScanner

SEHEMU YA KUMI

| Ada ya utumiaji wa machinjio na ukaguzi wa nyama | |
|---|---|
| 1. Ada ya utumiaji wa machinjio | Tshs. 3000 kwa ng'ombe na Shilingi 2000/ kondoo na mbuzi. |
| 2. Ada ya Ukaguzi wa nyama | Tshs. 2000 kwa ng'ombe, Tshs. 1000 kwa mbuzi na Tshs. 200 kila kuku |

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

| Ushuru wa nyumba za kulala wageni | | |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru kwa kila nyumba ya kulala wageni | Asilimia kumi (10%) ya malipo yanayofanyika kwa kitanda na malipo kufanyika sio zaidi ya tarehe 2 baada ya mwezi wa malipo |

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

| Ushuru wa mazao ya kilimo | | |
|---|---|---|
| 1. | Mazao ya biashara | Asimilia tatu (3%) ya bei ya kuuzia/kununulia |
| 2. | Mazao ya kilimo | Asimilia tatu (3%) ya bei ya kuuzia/kununulia |
| 3. | Mazao ya misitu | Asimilia tano (5%) ya bei ya kuuzia/kununulia |

SEHEMU YA KUMI NA TATU

| Ada ya zabuni | | |
|---|---|---|
| 1. | Zabuni ndogo zilizotangazwa | Shilingi 50,000/= |
| 2. | Zabuni kubwa zilitangazwa kuanzia Milion 50,000 | Shilingi 100,000/= |
| 3. | Nukuu za bei ngazi za chini za Halmashauri | Shilingi 10,000/= |
| 4. | Uteuzi wa awali (pre – qualification) | Shilingi 50,000/= |



Scanned by CamScanner

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ndogo ya 11)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFILILISHA KOSA

Mimi ………………………………………….. mwenye Namba ya Simu ……………………………………..ninakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………………………… ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kwamba mnamo tarehe ……. ya mwezi ……… mwaka ………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba za Mwaka 2020.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi, niko tayari kulipa kiasi cha shilingi………………………………………………………na kutimiza wajibu wangu chini ya Sheria Ndogo hiyo badala ya kushtakiwa Mahakamani.

leo tarehe…………………………ya Mwezi……………Mwaka……………..

Mbele ya;
Jina…………………………cheo……………………….
Saini……………………………………
Tarehe…………………………………..



Scanned by CamScanner

Nembo na Muhuri wa' Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia Azimio la Baraza la Madiwani lililofanyika tarehe 30 mwezi Mei Mwaka 2019 na ilibandikwa mbele ya :-

PENDO A. MALABEJA
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba*

MHE. PETER L. NGASSA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba*

NAKUBALI,

L.S

Dodoma,
1 Septemba, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB.),
*WN OR-TAMISEMI*



Scanned by CamScanner